TUKI
KAMUSI YA KISWAHILI-KIINGEREZA
Swahili-English Dictionary

TOLEO LA PILI

TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

2014

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
S.L.P. 35110
Dar es Salaam.

© Taasisi ya Taaluma za Kiswahili 2014
Toleo la Kwanza 2001, Chapa ya Pili 2004, Chapa ya Tatu 2006
Chapa ya Nne 2008, Chapa ya Tano 2010
Toleo la pili 2014

ISBN 9976 911 44 0

Haki imehifadhiwa, hairuihusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigisha chapa au kutoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

PL
8703
.T855
2014

DIBAJI YA TOLEO LA PILI LA KAMUSI YA KISWAHILI-KIINGEREZA

Kukamilika kwa Toleo la Pili la Kamusi hii ya Kiswahili-Kiingereza kumetokana na historia ndefu ya Toleo la Kwanza. Hivyo, itakuwa jambo jema ikiwa tutaanza kutoa usuli wa Toleo la Kwanza la kamusi hii. Wazo la kutunga Toleo la Kwanza la kamusi hii lilianzishwa mwaka 1964 na Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili (ambacho kuanzia mwaka 1972 kilijulikana kama Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, TUKI). Wazo hili lilibuniwa wakati wa uongozi wa Profesa Wilfred H. Whitely, ambaye ndiye alikuwa Mkurugenzi wa Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, ikiwa ni miaka 25 baada ya kuchapishwa kwa kamusi ya Johnson ijulikanayo kama *Standard Swahili-English Dictionary (1939)*. Kazi ya utunzi wa kamusi mpya ilianza baada ya shirika la *Calousse Gulbenkian Foundation* kutoa msaada wa pesa kwa Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 1964 hadi Oktoba 1967, ili kukiwezesha chuo kumwajiri mchunguzi atakayeweza kufanya kazi hiyo.

Katika kutekeleza azma hiyo, Chuo kilimwazima Bwana J.A. Tejani kutoka Wizara ya Elimu Zanzibar na kumwajiri kuwa Mchunguzi. Bwana Tejani wakati huo alikuwa na shahada ya kwanza ya Sanaa (B.A.) katika lugha za Kiarabu na Kiajemi ya Chuo Kikuu cha London, na alikuwa pia na ujuzi katika lugha za Kigujarati, Kiurdu na Kiswahili. Ilipangwa kuwa Tejani angekuwa anasaidiwa na Mchunguzi Msaidizi na pia angeshauriwa na Bi. M.A. Bryan wa *School of Oriental and African Studies (SOAS)* cha London, Prof. E. Damman wa *Marbury* na Prof. D.A. Olderogge wa *Leningrad*. Bwana Tejani, akiwa Mkurugenzi wa Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili kati ya mwaka 1968 na 1969, aliendelea kuifanya kazi hii hadi mwaka 1970 alipoikabidhi kwa Mkurugenzi mpya wa Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, Bwana George Mhina. Mwaka 1967, kabla ya kuteuliwa kwa Mkurugenzi mpya, Baraza la Kiswahili la Taifa lilikielekeza Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili kuwa kamusi inayopasa kuandaliwa kwanza iwe ni kamusi ya Kiswahili-Kiswahili na wala sio Kamusi ya Kiswahili-Kiingereza. Kwa hiyo, mwaka 1970 kazi ya kwanza ya Mkurugenzi mpya, Bwana George Mhina, ilikuwa ni kuhakikisha kuwa vitomeo vinatafsiriwa upya katika Kiswahili. Mswada wa kamusi ya Kiswahili-Kiswahili ulikamilika tarehe 4 Juni, 1978 na kamusi ikachapishwa mwaka 1981.

Mwaka 1972, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ilimpata mtaalamu wa kamusi kutoka Poland, Prof. Rajmund Ohly. Kwa kuanzia, Profesa huyu alipewa kazi ya kutunga kamusi ya Kiingereza-Kiswahili. Hata hivyo, mwaka 1975, Taasisi ilipounda jopo la wataalamu wa kamusi ili kukamilisha kazi ya kutunga kamusi ya Kiswahili-Kiswahili, Prof. Ohly alisitisha kazi ya kutunga

Dkt. G. Mrikaria - Katibu
Mussa M. Hans - Mjumbe
Musa M. Shembilu - Mjumbe
Arnold Gawasike - Mjumbe
Timothy Mapunda - Mjumbe
Elizeus G. Katikiro - Mjumbe
Titus Mpemba – Mjumbe

Baada ya majopo ya Kamusi yaliyofanyika mwaka 2011, mradi huu ulisimama hadi mwezi Machi, 2013 ambapo ulianza tena na kufanyika majopo mawili. Mnamo mwezi Juni, 2013 lilifanyika jopo jingine ambapo, Kaimu Mkurugenzi, Prof. Yohana P. Msanjila, alibaini kuwa kazi ya uhariri inachukua muda mrefu na akawaagiza wanajopo kupanga majopo ya mfululizo ili kuhakikisha kwamba kazi hii inakamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2013. Wanajopo walikubaliana na ushauri wa Kaimu Mkurugenzi na kufanya majopo manne mfululizo ambayo yalikuwa na mapumziko mafupi sana kati ya jopo na jopo, ili kuhakikisha kwamba kazi hii inakamilika kama ilivyopangwa. Majopo yote haya manne yalifanyika katika hoteli ya Njuweni iliyoko Kibaha kuanzia mwezi Septemba hadi Novemba, 2013.

Mbali na kazi nyingine, wakati wa uhariri, wanajopo walishughulikia semi, minyumbuliko ya vitenzi, kupitia maoni ya wasomaji mbalimbali na kuingiza maneno mapya ambayo waliona kuna umuhimu wa kufanya hivyo. Kwa hakika, kazi hii ya uhariri, haikuwa nyepesi hasa, ukizingatia kwamba mambo yaliyofanyika wakati huo ni mengi, hivyo iliwalazimu wanajopo wakati mwingine kufanya kazi usiku na mchana. Taasisi inawapongeza wanajopo kwa kazi nzuri na muhimu waliyoifanya. Majopo haya yalishirikisha wanajopo wafuatao:

Dkt. G. Mrikaria - Mwenyekiti
Dkt. E.K.F. Chiduo - Mjumbe
Mussa M. Hans - Mjumbe
Musa M. Shembilu - Katibu
Arnold Gawasike - Mjumbe
Timothy Mapunda – Mjumbe

Kukamilika kwa Toleo la Pili la kamusi hii kulitokana na ushirikiano na mchango kutoka kwa watu na makundi mbalimbali. Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa wataalamu mbalimbali waliotenga muda wao kusoma na kutoa maoni yao kwa Toleo la Kwanza la kamusi hii. Ingawa hatuwezi kuwataja wote kwa majina, litakuwa jambo jema tukiwataja japo wachache. Miongoni mwa wataalamu hao ni Prof. Irmtraud Herms, Prof. D.P.B Massamba, Sista Anita Macwilliam na Peter White. Aidha, tunaishukuru EMAC yenye dhamana ya kusimamia na kudhibiti ubora wa vitabu vya elimu, hususan katika ngazi ya msingi na sekondari.

Vilevile, tunapenda kutambua mchango wa wakurugenzi wa Taasisi waliotangulia wakati kazi hii ikiendelea katika hatua mbalimbali ambao ni Prof. M.M. Mulokozi, Prof. J.G. Kiango na Dkt. A.K. Mutembei.

Kwa kuhitimisha, tunatoa shukrani za pekee kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ukiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Rwekaza S. Mukandala, kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za TATAKI za kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa.

Profesa Yohana P. Msanjila
KAIMU MKURUGENZI
Machi, 2014.

kl	=	kielezi
(Kla)	=	Kilatini
(Kng)	=	Kiingereza
(Kre)	=	Kireno
(Kta)	=	Kiitaliano
kt	=	kitenzi
(Ktu)	=	Kituruki
ku	=	kiunganishi
kv	=	kivumishi
kw	=	kiwakilishi
(ms)	=	msemo
(mt)	=	methali
(nh)	=	nahau
nm	=	nomino
<sie>	=	sielekezi
taz	=	tazama

A,a

aa pia **ahaa** *ki* (kutegemea kiimbo) ah!

aalam* *kv* (Mungu pekee) the most knowledgeable: *Allahu ~* Almighty God, the most knowledgeable. *(Kar)*

aali* *kv* superior, great; exalted: *Haya ni mambo ~* these are great (exalted) things. *(Kar)*

aalimu* *nm* [*a-/wa-*] (ksh) 1 educated man in islamic knowledge. 2 scholar. ►*kv* having profound islamic knowledge. *(Kar)*

aathari* *nm* relic; ruins. *(Kar)*

abaa! *ki* hallo! hey!

abadani!* *ki* not at all, never: *Hutakubaliwa ~* you will never be accepted. *(Kar)*

abadi* *kl* forever, eternity, always, permanently: *Tatizo hili sasa ~* this is now a permanent problem. *(Kar)*

abakusi* pia **abaki** *nm* [*i-/zi-*] abacus. *(Kng)*

abedari* *nm* [*i-/zi-*] pulley used on dhows. *(Kar)*

abee! pia **bee**! *ki* (wanawake) word used in response to summons or address.

abiri[1]* *kt* *<ele>* sail, navigate, travel. (*tde*) **abiria** sail at some place/with sth/ because of; (*tdw*) **abiriwa**. *(Kar)*

abiri[2]* *kt* *<ele>* forecast; foretell; predict. (*tde*) **abiria**; (*tdk*) **abirika** can be predicted. *(Kar)*

abiri[3]* *kt* *<sie>* learn from experience or incidents. (*tde*) **abiria** learn from experience at some place; (*tdk*) **abirika**. *(Kar)*

abiria* *nm* [*a-/wa-*] passenger: *Garimoshi la ~* passenger train; *Gari la ~* bus; *Mizigo ya ~* passenger luggage. *(Kar)*

abjadi* *nm* [*i-/zi-*] alphabet: *~ ya Kiswahili* Swahili alphabet; *~ za Kirumi* Roman alphabet. *(Kar)*

ablauti* *nm* [*i-/zi-*] (sarufi) ablaut. *(Kng)*

abra* *nm* [*i-/zi*] chance, opportunity, spare time: *Sina ~* I have no time; *Sijapata ~ ya kuongea nao* I haven't had an opportunity to talk to them. *(Kar)*

abtali* *nm* [*wa-*] heroes, heroine. *(Kar)*

abu* *nm* [*a-/wa-*] (ksh) father. *(Kar)*

abud.u[1]* *kt* *<ele>* 1 worship: *~ Mungu mmoja* worship one God. 2 idolize. 3 adore, love: (*nh*) 1 *~ kazi* adore work. 2 *~ usingizi* adore sleep. (*tde*) **abudia** worship at some place/because of; (*tds*) **abudisha** cause sb to worship; (*tdw*) **abudiwa** be worshiped. *(Kar)*

abudu[2]* *nm* [*a-/wa-*] toy. *(Kar)*

abunusi* *nm* [*u-/i-*] (ksh) ebony: *Samani za ~* ebony furniture. *(Kar)*

abunuwasi* *nm* [*a-/wa-*] cunning character in Arabic tales. *(Kar)*

aburani *nm* [*i-/zi-*] (ksh) pledge.

abuwabu* *nm* [*zi-*] (ksh) doors: *~ ziko wazi* the doors are open. *(Kar)*

abwe! pia **ebo**! *ki* wow!

abyadhi[1]* *kv* white: *Shati ~* a white shirt. *(Kar)*

abyadhi[2]* *nm* [*i-*] (ksh) playing card or dice which has no number on it. *(Kar)*

ach.a[1] *kt* *<ele>* 1 quit/stop doing sth, recant, desist: *~ ulevi* quit/stop drinking; *~ kazi* quit job; *~ kukohoa* stop coughing. 2 leave behind: *Wasafiri wame~ mizigo yao nyuma* passengers left their luggage behind. 3 abandon, discontinue, neglect, chuck in, come away, discard, desert: *Watu wame~ mashamba yao* people have neglected their farms; *Kuku ame~ watoto wake* the hen has deserted her chicks. *~na*